



BODI YA KAHAWA TANZANIA

TAARIFA KWA UMMA

KUANZA KWA MINADA YA KAHAWA MKOANI KAGERA TAREHE 07/06/2022

Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) inawatangazia wadau wote wa kahawa kuwa itaendesha mnada wa kwanza wa kahawa Mkoani Kagera siku ya Jumanne tarehe 07/06/2022 kuanzia saa 05:00 asubuhi.

Mnada huu utafanyika kwa njia ya mtandao (Online) ambapo wanunuzi wenye leseni wataweza kushiriki wakiwa sehemu yoyote ndani ya Tanzania na pia kushiriki mnada kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba. Pia wadau wengine wanaruhusiwa na wanaweza kufuatilia mwenendo wa mnada huo katika ukumbi huo.

Aidha, Bodi inawataka wanunuzi wengine leseni na nia ya kushiriki katika minada kuweka amana ya Shilingi Milioni 10 kwenye akaunti ya Bodi **01J1038896702 Iliyoko CRDB Bank (Jina Tanzania Coffee Board)** pamoja na kutekeleza matakwa mengine kama ilivyoelekezwa katika mwongozo Na. 1 wa usimamizi wa masoko ya kahawa kwa msimu wa 2022/2023.

Kabrasha la mnada (Sales Catalogue) litapatikana katika tovuti ya Bodi ya Kahawa www.coffeeboard.or.tz pamoja na kutumwa kwenye barua pepe za wanunuzi,

Wanunuzi watakaohitaji msaada zaidi wawasiliane nasi kupitia namba +255 754289167 na +255 713298314

Kajiru F. Kisenge

Kny. KAIMU MKURUGENZI MKUU

